

KITUO CHA HABARI ZA MAENDELEO TANZANIA (TDIC)

Maelezo kuhusu TDIC

Kituo cha Habari za Maendeleo Tanzania (TDIC) ni mpango wa kuhamasisha ubia wa mashirika ya nchi mbili au zaidi, unaoendeshwa na Kituo cha Tanzania cha Mafunzo ya Maendeleo ya Dunia (TGDLC) kilichopo Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM). TDIC imeanzishwa ili kuhamasisha matumizi na upatikanaji wa habari ili kuboresha ufanisi wa programu za maendeleo nchini Tanzania. Kwa kutumia rasilmali za kituo, wanafunzi, umma, watafiti na watunga sera wanaweza kupata taarifa mbalimbali kuhusu maendeleo.



- **Majadiliano ya Maendeleo:** Mashirika au asasi za maendeleo zinazoendesha majadiliano kuhusu maendeleo zinaweza kukodisha suhula za TDIC na kuwasiliana na wadau mbalimbali kupitia Kituo cha Tanzania cha Mafunzo ya Maendeleo ya Dunia (TGDLC).



- **Vitabu na Maonyesho:** Wadau wa Maendeleo wanaweza kuuza machapisho yao kwa mali kauli, kutoa mchango wa vitabu, CD-ROM na Video kwa ajili ya maktaba, au kutoa vipeperushi vyao kwa ajili ya kusambaza bure, na wanaweza kuweka maonyesho yao katika sehemu za maonyesho za TDIC.



Huduma za TDIC

- Maktaba ya wazi kwa ajili ya marejeo/ Maktaba iliyoshehenezwa machapisho ya maendeleo kuhusu Tanzania.
- Upatikanaji wa taarifa zinazohusiana na maendeleo katika Mtandao kwa kutumia kompyuta za kituo.
- Kuunganishwa na kazi za umma na mitandao inayohusiana na maendeleo.
- Upatikanaji wa machapisho ya wadau wa maendeleo.
- Upatikanaji wa machapisho kwa ajili ya mashirika ya ndani.
- Nafasi kwa ajili ya maonyesho.
- Ukumbi wa majadiliano ya maendeleo



Jinsi ya kushirikiana na TDIC

TDIC inashirikiana na watu binafsi, vikundi na asasi, kwa njia mbalimbali:

- **Mchango wa moja kwa moja:** Wadau wa maendeleo wenye nia ya kuhamasisha maarifa na taarifa kwa ajili ya maendeleo wanaweza kutoa michango ya fedha taslimu au mali kusaidia gharama za uendeshaji wa Kituo.



Hifadhi ya Nyaraka:

Kituo kinatoa taarifa kuhusu shughuli za mashirika rasmi ya maendeleo na wadau wengine wa maendeleo wanaofanya kazi Tanzania kikiwa ni kituo cha kutoa machapisho ya taarifa zao kwa umma.

Hifadhi kubwa ya vipeperushi na vijitabu vyenye mikakati ya misaada, sera za sekta, mihtasari ya miradi na ripoti za mwaka na hifadhi inaendelea kuboreshwa kwa taarifa kuhusu wadau wa maendeleo wa nchi mbalimbali na hasa nchini Tanzania.

Maktaba

Kituo cha Habari za Maendeleo Tanzania ni kituo kinachotoa huduma za marejeo kilicho wazi kwa umma wote unaohitaji taarifa kuhusu maendeleo nchini Tanzania, hususani watoa maamuzi, wanataaluma, waandishi wa habari, wabunge, vijana na watafiti.



Kituo pia huendesha majadiliano mbalimbali kwa ajili ya maendeleo na mada zinazohusiana na maendeleo katika ukumbi wake wa mikutano uliosheheni vifaa vya kisasa vya kuendesha mikutano. Machapisho katika kituo yanaweza kupatikana/kutafutwa kwa mtandao na kwa kutumia programu ya katalogi kwa ajili ya kupata kwa urahisi machapisho yaliyopo.

Kutumia Mtandao

Huduma ya mtandao kwa kutumia kompyuta tano za kituo inatolewa kwa umma ili kupata taarifa za maendeleo, kazi mbalimbali na taarifa nyingine zin zohitajika kwa ajili utafiti.




Ushirikiano na TDIC

TDIC imepata ushirikiano wa awali kutoka serikalini, wadau wa maendeleo na mashirika yafuatayo:

- Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO-PSM)
- Kanada, Serikali ya Kanada (CIDA)
- British Council
- Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM)
- Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC)
- Taasisi ya Utafiti wa masuala ya kiuchumi na kijamii (ESRF)
- Tanzania Chamber of Commerce Industries and Agriculture (TCCIA)
- Kituo cha Tanzania cha Mafunzo ya Maendeleo ya Dunia (TGDLC)
- United Nations, Education, Scientific and Cultural Organization (UNESCO)
- Benki ya Dunia

Ramani ya mahali TDIC ilipo



TDIC inatoa huduma kwa umma kama ifuatavyo:

Jumatatu-Ijumaa Kuanzia saa 3.00 asubuhi - 10.00 jioni
Jumamosi, Jumapili na Siku za Sikukuu: Haifunguliwi na kunaweza kuwepo mabadiliko bila kutoa taarifa.

Kituo cha Mafunzo ya Maendeleo ya Dunia Tanzania

IFM Block A, Sakafu ya Mwanzo,
Barabara ya Shaaban Robert,
S.L.P. 3918,
Dar es Salaam,
Tanzania.

Simu: +255 22 2123705/09

Fakisi: +255 22 2123702

Tovuti: www.tdic.or.tz




Kituo cha Habari za Maendeleo Tanzania

kilichopo katika

Kituo cha Mafunzo ya Maendeleo ya Dunia Tanzania (TGDLC)

IFM



www.tdic.or.tz



Tanzania Development Information Centre